



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI BILIONI 1.57 ZA UJENZI  
WA MIUNDOMBINU YA SHULE KUPITIA MRADI WA BOOST**

Taarifa inatolewa kwa umma kuwa Halmashauri ya Manispaa ya imepokea kiasi cha **Tshs. 1,574,900,000/=** fedha kutoka Serikali Kuu, ikiwa ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na awali kupitia mradi wa **BOOST** katika shule **saba** za Manispaa ya Ilemela.

Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1.08** zitatumika kujenga **shule mbili mpya za msingi zenye mikondo miwili, Shilingi milioni 400** zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa **vyumba 16** vya madarasa katika shule **nne** za msingi, **Shilingi Milioni 69.1** zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa **vyumba viwili vya madarasa ya mfano elimu awali**, na **Shilingi Milioni 25.2** zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa **matundu 12 ya vyoo** katika **shule 4 za msingi**

Shule za Msingi saba ambazo zimepokea fedha hizo ni pamoja na Shule ya **Buswelu, Chasubi, Igombe, Kahama, Nyamadoke, Nyamhongolo na Nyamwilolelwa.**

Utekelezaji wa Mradi wa **BOOST** unatarajiwa kuboresha kiwango cha elimu na fursa za upatikanaji wa elimu kwa watoto wa elimu ya awali na msingi Tanzania Bara. Sambamba na uboreshaji wa miundombinu, kuinua ubora wa walimu wa shule za awali na msingi na usimamizi na utawala bora katika utoaji huduma ya elimu.

**Violencea S. Mbakile**  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**  
**27 Aprili, 2023**

---

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,  
Tovuti: www.ilemelamc.go.tz